



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBINGA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na. MDC/I.20/21/VOL.II/18

09 Januari, 2024

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI AJIRA YA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbanga anapenda kuwatangazia nafasi za ajira ya mkataba kwa miezi mitatu kwa Watanzania wenye sifa kama ifuatavyo:-

Nafasi inayotangazwa ni:-

MKUSANYA USHURU (Nafasi Mbili)

i. SIFA ZA MWOMBAJI:

- ✓ Mwombaji lazima awe raia wa Tanzania
- ✓ Awe tayari kufanya kazi kwenye stendi ya mabasi ya Kiamili
- ✓ Awe na akili Timamu
- ✓ Awe mwadilifu.
- ✓ Awe na kitambulisho cha Taifa (NIDA, cha Mpiga kura, au utambulisho wa Serikali ya Kijiji.
- ✓ Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 48
- ✓ Awe na uwezo wa kutumia simu janja
- ✓ Awe amemaliza kidato cha Nne na kufauli, wenye elimu zaidi watafikiliwa
- ✓ Mwombaji aambatanishe vyeti vya Taaluma na picha tatu za rangi.
- ✓ Awe na wadhamini watatu wenye mali zisizohamishika.
- ✓ Asiwe mwajiri wa Serikali

ii. KAZI NA MAJUKUMU:

- I. Kukusanya mapato katika kituo atakachopangiwa.
- II. Kutunza kumbukumbu za risiti atakazo benk makusanyo ya siku husika na .
- III. Kutunza vizuri mashine ya kukusanya mapato (POS) na vifaa vingine atakavyokuta mahali pakufanyia kazi.
- IV. Kuwasilisha makusanyo katika akaunti ya Halmashauri .
- V. Kufanya kazi zote atakazopangiwa na msimamizi wake.

iii. MSHAHARA:

Mshahara wa Kukusanyaji Mapato ni 20% ya makusanyo kwa mwezi.

iv. MASHARTI KWA UJUMLA

- Mwombaji awe na wadhamini watatu wenye mali zisizohamishika.
- Maombi yaambatane na nakala za vyeti vya elimu
- Mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa.
- Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 16.01.2024 saa 9:30 Alasili.
- Barua zote zitumwe kwa anwani iliyopo hapo chini:-
- Barua zote zitakazotumwa kwa mkono hazitapokelewa.

Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
Halmashauri ya Wilaya Mbinga,
224Barabara ya Mbambabay,
S.L.P. 194,
KIGONSERA, RUVUMA.

NB: Tangazo hili pia linapatikana kwenye tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ambayo ni:- www.mbingadc.go.tz



Juma Haji Juma
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MBINGA